**SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO**

**MKATABA Na. 2**

# MKATABA WA UPANGAJI NA UKARABATI WA JENGO NAMBA SIDO/ARA/BLG/16

**(KAMPUNI)**

***BAINA YA***

**SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO (SIDO)**

***NA***

**M/S** IMARA TECHNOLOGY CO. LTD

**SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO**

**MKATABA Na. 2**

**MKATABA WA UPANGAJI NA UKARABATI**

**MKATABA HUU** umesainiwa leo tarehe **15** Mwezi Febrari **2021**

***BAINA YA***

***SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO***, Shirika lililoundwa chini ya Sheria ya Bunge Na. 28/1973 S. L. P. ARUSHA (ambalo katika mkataba huu litajulikana kama "Mmiliki") kwa upande mmoja,

***NA***

**IMARA TECH-ARUSHA** (ambaye atajulikana kwenye mkataba huu kama "Mpangaji") kwa upande mwingine.

**1.0 UTANGULIZI**

**KWA KUWA** SIDO ni mmiliki halali kisheria wa kiwanja **Na. 85** (hati ya umiliki Na. **12949** ya tarehe **12** Mwezi **DECEMBER** Mwaka **1990**
Kitalu E kilichopo **UNGA INDUSTRIAL AREA**

**KWA KUWA** Mpangaji anahitaji eneo la kufanyia biashara ambapo atakarabati jengo kufuatana na michoro iliyoidhinishwa na **SIDO** kwenye jengo lililoko katika Mtaa wa **UNGA LTD** uliotajwa na amekubali kuchukua eneo hilo kwa ajili ya kufanya biashara ya **KUZALISHA MASHINE NA VIFAA VYA TEKNOLOJIA AINA MBALIMBALI.**

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:**

**2.0 TAFSIRI NA UFAFANUZI**

2.1 Mkataba maana yake ni mkataba huu wa upangaji na ujenzi

2.2 Mpangaji maana yake ni **IMARA TECH LTD** ambapo neno mpangaji litatafsiriwa pia kumaanisha mjenzi.

2.2 Mmiliki maana yake ni SIDO ambapo tafsri yake itajumuisha SIDO pamoja na warithi wake wote halali

2.3 Notisi maana yake ni mawasiliano maalum ya kimaandishi kati ya mpangaji na mmiliki yatakayotolewa kwa mujibu wa mkataba huu.

2.4 SIDO maana yake ni Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo ambalo katika mkataba huu ndio mmiliki.

**3.0 UHALALI WA MKATABA**

3.1 Mkataba huu utaanza tarehe **15** Mwezi **FEB** Mwaka **2021** na utamalizika tarehe **15** Mwezi **JANUARY** Mwaka **2022** baada ya muda huu mkataba utarejewa tena.

3.2 Mkataba huu hautatafsiriwa kuwa halali ikiwa haujatiwa saini na pande zote mbili.

3.3 Mkataba huu utarejewa kila baada ya **MWAKA MMOJA** na kusainiwa upya na pande zote.

3.4 Mkataba huu ukimalizika muda wake, au wakati wa marejeo baada ya kipindi cha **MWAKA MMOJA** unaweza kurejewa kwa makubaliano kama haya au kwa makubaliano mengine.

**4.0 MASHARTI YA MKATABA**

4.1 Mpangaji atakarabati kwa gharama zake mwenyewe jengo la gharama isiyozidi Sh.TSH **5,246,150/= [SHILINGI MILIONI TANO LAKI MBILI AROBAINI NA SITA ELFU NA MIA MOJA HAMSINI TUU ]**

4.2 Gharama za ukarabati wa jengo hilo zitahakikiwa na SIDO kama gharama halisi zilizotumika au zitakazotumika.

4.3 Ukarabati wa jengo utaanza tarehe **15/11/2020** na utatakiwa uwe umekamilika kufikia tarehe **15/02/2021**

4.4 Kodi ya upangaji itaanza rasmi kutozwa ifikapo tarehe **15/02/2021** mara baada ya ujenzi kukamilika.

4.5 Mpangaji atailipa SIDO Shilingi za Tanzania **156,250** kwa miezi kumi na moja kuanzi mwezi February 2021 hadi mwezi December 2021 na Tsh **535,100/=** kwa mwezi mmoja ambao ni mwezi **January 2022** zikiwa ni asilimiia **25%** ya kodi ya kupanga eneo hilo la biashara.

4.6 Mpangaji atabaki na asilimia **75%** ya kodi halisi ya pango kama gharama ya kufidia ujenzi wa jengo sawa na shilingi za kitanzania **5,246,150/=** Fedha hizi zinatarajiwa kulipwa kwa kipindi cha miezi kumi na mbili.

4.7 Viwango vya kodi ya pango vitaweza kufanyiwa marekebisho wakati wa marejeo ya mkataba na kodi itaweza kupanda au kushuka kutegemeana na kupanda na kushuka kwa thamani ya fedha. Viwango vipya vya kodi vitakavyopendekezwa na SIDO vitapaswa kutumika.

4.8 Mpangaji hataruhusiwa kuhamisha upangaji wa eneo au sehemu ya eneo alilopangishiwa kwa mtu mwingine bila idhini ya maandishi ya SIDO.

4.9 Wakati wote wa uhai wa mkataba au baada ya kwisha kwa mkataba, Mmiliki hatahusika kwa namna yeyote kulipa, kufidia au kuchangia hasara au athari yoyote dhidi ya binadamu, mazingira au vinginevyo, iliyosababishwa na shughuli yeyote ya mpangaji katika eneo alilopanga au matokeo ya shughuli zake zilizofanyika ndani ya pango lake.

4.10 Wakati mkataba wa upangaji unaendelea, endapo itatolewa amri halali ya kisheria ya kubomoa jengo na Mamlaka yoyote halali, Mpangaji atabomoa jengo kwa gharama zake mwenyewe katika muda atakaopewa.

4.11 Mpangaji ataingiza umeme na maji kwenye jengo na pia ataweka mita ya umeme kwa gharama zake mwenyewe.

4.12 Miezi mitatu kabla ya mkataba kumalizika / kabla ya kipindi cha marejeo kufika, Mpangaji ataandika barua kwa Meneja wa Mkoa wa SIDO kuomba kuendelea na mkataba kwa kipindi kingine. Asipofanya hivyo itahesabika kuwa mkataba ukimalizika hatapenda kuendelea na mkataba kwa kipindi kingine.

4.13 Mpangaji anaahidi kuendesha biashara yake kiustaarabu bila kuwabughudhi Wapangaji wengine au majirani na atahakikisha anafanya biashara iliyoelezwa kwenye mkataba huu tu. Ikiwa atataka kubadili aina ya biashara itambidi kupata kibali cha maandishi cha SIDO.

## 5.0 USITISHWAJI WA MKATABA NA MATOKEO YAKE

5.1 Kila upande unaweza kukatisha mkataba kwa kutoa notisi ya maandishi ya mwezi mmoja ikielezea sababu za kutaka kukatisha mkataba.

5.2 Mkataba ukiisha na Mpangaji kuamua kuondoka, Mmiliki hatamlipa Mpangaji kwa maendelezo yoyote (unexhausted improvements) atakayokuwa amefanya kwenye eneo kama hakuna makubaliano ya maandishi na SIDO kuhusu kurejesha gharama.

5.3 Mpangaji atalazimika kutumia jengo atakalojenga wakati wote wa mkataba huu na kama ataacha kulitumia au atalitelekeza kwa muda wa miezi mitatu Mmiliki ana haki ya kumtaka kulivunja na kuondoka ili eneo lipewe mfanyabiashara mwingine anayehitaji.

5.4 Mpangaji atahusika na gharama za uzoaji taka na usafi katika eneo alilopanga.

**KAMA USHUHUDA** mkataba huu umetiwa saini na pande zote tarehe, mwezi na mwaka uliotajwa hapo juu.

IMEPIGWA MUHURI wa SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO na KUTOLEWA mbele yetu leo tarehe 15 mwezi **FEBRUARY** mwaka 2021.

Saini........................................

Jina...HONEST J. MTUI

Anuani .......1278- ARUSHA

Wadhifa KAIMU MENEJA WA MKOA

Saini........................................

Jina....ANITA N. MERO

Anuani....1278 - ARUSHA

Wadhifa..MHASIBU WA MKOA

Muhuri wa Shirika

(S. I. D. O)

Tar. 15/2/21

IMEPIGWA MUHURI wa IMARA TECH LTD na KUTOLEWA mbele yangu leo tarehe 15 mwezi **FEBRUARY** mwaka 2021

Saini........................................

Jina......ALFRED B. CHENGULA

Anuani .........1763, ARUSHA

Wadhifa ...MKURUGENZI MTENDAJI

Muhuri wa Kampuni

P.O. Box 1763 ARUSHA

**Mbele yangu;**

Saini........................................

Jina......Jane J. Mwambegele

Anuani.......75156 DSM

Wadhifa ....Wakili